# Tutakuwa na furaha kama...
# tutapenda **haki**

"Heri wenye njaa na kiu ya haki maana hao watashibishwa" (Mt 5,6)

## Lengo

Tutambue uwezekano wa kujituma kibinafsi na kama kundi, katika kutekeleza haki katika ngazi ya dunia nzima.

## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mangámuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"

## Shughuli ya utambulisho

### « UKOSEFU WA HAKI DUNIANI »

**MUDA:** kama dakika 45

**VIFAA:** ramani ya dunia (picha au fotokopi), magazeti/ majarida au simu ya mkononi/kijidaftari, kalamu nyekundu au rangi

**UENDESHAJI:** Mnakili au mchore ramani ya dunia, halafu kwa msaada wa habari za magazetini na kwenye tovuti, pakeni rangi nyekundu nchi ambazo haki imekadamizwa wazi wazi kwa sababu ya vita, udikteta, kutokana na ukosefu wa chakula, wa maji...eneo jekundu lina ukubwa gani ukilinganisha na eneo jeupe? Mnaweza kusema nini juu ya hiyo hali? Mnaweza kufanya mahojiano ili kujua maoni ya wazazi, ndugu, wapitanjia, wafanya biashara wa mtaani kwenu, wataalamu.

**HITIMISHO:** Tutenge muda wa mazungumzo kwa kuuliza maswali kadhaa. Kitu gani kipya tulichojifunza kutokana na shughuli hii? Ni kwa kiasi gani mchango wa kila mtu ni wa muhimu ili kutimiza haki duniani?

## Tuishi hivi

Mwaka huu nilipata alama ya juu sana iliyonifanya nistahili kupata “scolarship” ambayo mwishoni mwa mwaka viongozi wa chuo hutoa kwa wanafunzi wa ‘kwanza’ wa kila darasa. Lakini niligundua kuwa mwanafunzi mwenzangu aliyekuwa wa pili hakustahili kupata ‘scholarship’ lakini alihitaji zaidi yangu. Bila huo msaada asingeweza kuendelea na masono na tena mama yake alishaamua kumuondoa shuleni. Mimi, kama gen 3, nilijifunza kuishi kwa ‘msaada’ amabo ulinisaidia daima: ulikuwa wakati wa kumpenda mwanafunzi mwenzangu kimatendo, ilikuwa haki zaidi kwake kupata zile pesa. Hivyo nilienda kwa mwalimu mkuu kupendekeza mabadilishano: mimi kuchukua nafasi ya pili na kumpa nafasi ya kwanza yule mvulana. Kila kitu kilitakiwa kufanywa kwa siri ili watu wasigundue hilo. Mwalimu mkuu alikubali. Mwishowe nilifurahi kupata uwezekano wa kumpenda Yesu ndani ya yule mwanafunzi mwenzangu aliyehitaji zaidi na nafasi ya kujenga naye umoja. Hamuwezi kufikiri furaha yangu, wakati wa kujisajili kwenye kozi iliyofuata, baba yangu, bila kutarajia, alipata ‘msaada’ haswa kwa ajili ya masomo yangu!

*(E. – Colombia)*



Tutakuwa na furaha kama... **tutapenda haki**

## Kwa undani

### «ILI KUPATA MARA MIA»

Yesu asema: ‘heri wenye usafi wa moyo maana watamona Mungu’, lakini watu wengi wanasema kuwa kwa uwongo, udanganyifu na kwa rushwa wanapata zaidi, hasa wanapata pesa nyingi, nyingi zaidi kuliko kwa haki. Chiara, ni ushauri gani unaweza kutupatia?



Mimi nasema kwa ukweli kwamba wale wanaotaka pesa, wanaojishughulisha ili kupata pesa nyingi hawana bahati ya ziada. Inatosha kuangalia kwa mfano, tajiri: alienda motoni wakati Lazaro, aliyekuwa masikini alienda Paradiso, hivyo alikuwa mwenye bahati zaidi. Wema wa kweli haupo katika kuwa na mali nyingi, wema wa kweli upo katika kupenda na katika haki. Sisi tunapaswa kufanya hivi. Ninyi mtasema: kwa hiyo tutakuwa masikini milele? Si kweli! Injili inasema: “ tafuteni kwanza ufalme wa Mungu – maana yake: jitajidini kupenda – na mengine mtapewa kwa ziada”, ni Msaada unaofika. Kwa hivyo, tutapata mali nyingi mara mia hapa duniani. Na halafu maisha ya milele.

***Chiara Lubich, Castelgandolfo, 22.6.2000 – Kongamano la gen 3 wasichana na wavulana wa miaka 9-12 – n°5***

# «DHIDI YA NJAA, TUBADILISHE MAISHA»



*Luigino Bruni (mwanauchumi),*
*Kongamano la gen 3 wasichana.*
*(13/17 a.), Castelgandolfo,*
*3 februari 2005*

Tunajua kwamba tatizo kubwa kwa nchi zinazoendelea ni usambazaji wa mali usio wa haki. Tunawezaje kuelimisha watu ili kuboresha hali hii? Na juu ya yote, jinsi gani tunaweza kufanya ili kusaidia nchi hizo masikini?

Mimi naamini kuwa umaskini utaondolewa kama matajiri watabadilisha maisha yao. Dunia haiwezekani bila umaskini unaozalishwa, hausababishi mabadiliko ya matajiri kupunguza utajiri. Hii haiwezekani. Kama dunia tajiri itaendelea kuwa kama ilivyo, haitoi, kama haitoi mali zake ili kuwasaidia maskini, umaskini hautatatuliwa kamwe . litakuwa tatizo la kejeli siku zote, ni hotuba inayoendela kwa miaka 50 na juu ya yote inakuwa mbaya zaidi. Kwa kweli, katika baadhi ya maeneo ya dunia hali inazidi kuwa mbaya baada ya miaka 50 ya misaada kwa umaskini. Kwa nini? Kulikuwa na kaulimbiu nzuri sana miaka iliyopita, ambayo ninawapendekeza tena: "Kupambana na njaa, badili maisha." Ina maana kwamba kama hubadilishi maisha, yaani kama huwi na kiasi, mlaji wa kiasi, njaa, umaskini, havitaisha kamwe. Ni ndoto, ni udanganyifu kufikiri, yanabaki maneno tu mazuri.

Hivyo, kupambana na umasikini, maisha yanabadilika,... lakini inabidi kuyabadili pamoja na wengine. Tukitaka kuathiri ulimwengu wa wenye nguvu, wale wanaofanya maamuzi makubwa, tunapaswa kuwa pamoja na kuchukua hatua pamoja na watu wengine. ... Baadhi ya malengo makubwa yanakamilika kwa sababu tunaungana na watu wengine. Hii ina maana kwamba, kwa mfano, tuwe marafiki na wale vijana wote wanaoishi kwa ajili ya ulimwengu wenye haki zaidi, na ni wengi, au kuhudhuria warsha za biashara ya haki. Kuwa na mshikamano na watu hawa, wakati mwingine nunua kitu kutoka kwao, halafu kuwa na mtandao na wale ambao wanaishi kwa ajili ya dunia bora na wao ni wengi. Si wachache vijana wanaoishi kwa ajili ya ulimwengu bora, kwa sababu kwa kweli peke yetu kwa aina hii ya mapambano ya kijamii - katika maana nzuri ya neno - haiwezekani kushinda. Hata sisi wa Movement, peke yetu, hatuwezi, kwa sababu tatizo la umasikini ni kubwa mno. Wakati watu wazima wanashirikiana pamoja na wengine wengi, kwa njia ya Uchumi wa Ushirika, hata ninyi vijana, ili muwe wengi, mnaweza kufanya urafiki na wale ambao tayari wanaishi hivi.



Tutakuwa na furaha kama... **tutapenda haki**

## Tutajaribu!

Ili kuifahamu zaidi hiyo mada hata pamoja na chipkizi wengine mnaweza kumtembelea mwekezaji katika kampuni ya Uchumi wa Ushirika. Je, mnamjua moja? Jaribuni kuwasiliana naye kisha pangeni hii shughuli ili kuwahamasisha chipkizi wa umoja wa mji wenu.

Mtazamo wetu unaweza kuvuka mipaka ya mji wetu ili kufanya chembe za haki hata na anayeishi katika mabara mengine. Hapa kuna pendekekzo la kutekeleza:

- Chagua mradi TEENS FOR TEENS na jambo halisi la kufanya ili kuutegemeza. Habari zaidi zipo katika wavuti wa AMU (Associazione Mondo Unito)

  ***http://www.amu-it.eu/wp-content/uploads/2015/11/2016-Progetti-AMU-Teens.pdf***





## Tupo katika hatua gani?

*Kufikia **lengo lazima** kufanya mazoezi kila siku na kutambua mabadiliko mazuri na magumu yaliyojitokeza. Itatusaidia mpaka mkutano ujao, wakati tutatenga muda wa kushirikashana mang'amuzi.*

Tulifaulu kuungana na watu wengine wanaoishi kwa ajili ya dunia iliyo na haki zaidi?

Nilipata nafasi gani ili kuwafahamu au kuwashirikisha wengine?

Nilimshirikisha nani?

Ni hatua gani tuliyoichagua ya kuitekeleza kwa pamoja?

Kwa ajili ya mlezi

## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza haki?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Nini ni muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?

Tutakuwa na furaha kama... tutapenda haki